

Jiwe la kujengea la Kiroho 4.

## MSALABA INABIDI UKUMBUKWE KILA SIKU

***Yohana Mtakatifu 19:30 “Yesu alisema umekwisha”***

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo kalvari inabidi ikumbukwe kila siku.

Tumesikia mengi kuhusu hiyo, Tumesema mengi juu ya hiyo, Wahubiri wamehubiri kuhusu hiyo tangu mwanzo wa wakati, Waimbaji wameimba kuhusu hiyo tangu miaka na miaka. (Katika nyakati zote ) Manabii wamethibitisha miaka elfu nne kabla ya kule kutokea kwake (***Zaburi 22:1-18, Isaya 50:6, 53:1-12***) na manabii wa leo wanaelekeza nyuma pale ilipotendeka.

Ni siku ya muhimu mno kuzitupa hapa Duniani. Kama hii siku ni ya muhimu sana moja ya siku kuu mno. Hebu tuangalie mambo matatu tofauti ambayo tuende kwa hayo hiyo siku ilimaanisha ni kwetu. Tunaweza kuchukua vitu zaidi ya mia. Lakini nimechagua vitu vitatu tofauti vya muhimu ambavyo tunaenda kuviangalia katika muda mfupi Kalvari ilimaanisha kwetu. Nami ninaomba kwamba nitamhukumu kila mwenye dhambi aliyeko hapa, nitamfanya kila mtakatifu apige magoti. Nitawafanya kila mtu aliye mgonjwa ainue imani yake kwa Mungu na asiondoke atembe akiwa ameponywa, kila mwenye dhambi aokolewe, kila aliyerudi nyuma arudi na ajionee aibu haya yeye mwenyewe, naalika Mtakatifu afurahi na kuchukua mtazamo mpya na matumaini mapya.

Lile jambo kuu la muhimu ambalo Kalvari ilimaanisha kwetu na Dunia nzima, ni kuwa ilimaliza swali la dhambi kwa mara moja na kwa nyakati zote (***1Yohana:1-9, 5:18***) mtu alipatikana nahatia ya dhambi ilihitaji adhabu ambayo hakuna mtu ambaye angeweza kuilipa (***Rumi 3:23-27***). Ile adhabu ilikuwa ni kubwa sana kiasi kwamba hakukuwa na mtu yoyote ambaye angelipata naamini Mungu aliweka hilo liwe hivyo kwamba ile adhabu ingekuwa kubwa kiasi kwamba hakuna mtu angeweza kuilipa hiyo, ili yeye mwenyewe aweze kuilipa, (***Isaya 53:3-4, Ebrania 2:14-16***) sasa mshahara wa dhambi ni mauti (***Warumi 6:23***) na sisi sote tumezaliwa katika dhambi. Tumeumbwa katika uovu, kwa hiyo hakuna hata mmoja wetu ambaye amestahili, wala wasingeweza kumpata hata mmoja duniani ambaye angestahili (***Ufunuo 5:1-5***). Na dhambi haikuanza hapa Duniani, dhambi ilianza Mbinguni Lusiferi yule Shetani alikuwa ni kiumbe aliyelaaniwa kwa sababu ya kutotii kwake kabla hajaja Duniani dhambi ilianza mbinguni ambapo Mungu aliwaweka malaika katika msingi uleule ambao aliwaweka wanadamu. Ule mti wa uzima, ni mti wa maarifa, ambapo mwanadamu angefanya

uchaguzi wake, (**Mwanzo 2:15-17**). Na wakati lisiferi alipopewa utangulizi afanya uchaguzi wake alitaka kitu kizuri zaidi ya Mungu alichokuwa nacho. Hilo lilianzisha matatizo.

(**Isaya 14:12-15, Ezekieli 28:11-17**)

Kwanza tutafute tuone ile siku ilimaanisha nini pili tunapaswa tuone ni kitu gani ile siku ilitufanyia sisi. Sasa, 3, hebu tuangalie kile tuwezacho kufanya kwa ajili ya siku ile, tunapaswa kufanya nini.

Kwanza tunapaswa kuangalia hilo, kwa maana ni siku kuu, sikukuu kuliko zote. Gharama ya dhambi ililipwa. Nguvu za shetani zilivunjwa (**Kolosai 2:13-15, Mwanzo 3:15**)

Na sasa, tuone kile tupaswacho kufanya kwa ajili yake. Sasa kwa ajili yake, ni pale yesu alipokufa msalabani siku ile. Pale Kalvari siku ile yeye sio tu kwamba alilipa gharama ya dhambi kwa ajili ya dhambi zetu, lakini alilipa ile gharama na kutengeneza njia kwamba tunaweza kumfuata yeye (**Waebr 10:19-23**) kwa kuwa sisi kama adamu aliyeanguka ambaye amekombolewa, kama roho alivomoungoza Adamu, Yule adamu wa kwanza kwa Roho Yule ambaye anatawala vitu vyote vya asili..... (**1Kor 15:45-50**). Sasa sisi watu waduniani tumekombolewa na Kristo tangu siku ile pale Kalvari tunaweza kumfuata yeye.

Hivyo ndivyo Kalvari ilimaanisha kwako katika njia kuu (**Isaya 35:8**) ilifunguliwa siku ile kwaajili yako. Sasa, alipokufa pale Kalvari au Msalabani alitengeneza njia alitoa Roho yake, yule Roho Mtakatifu ambaye alimtuma nyuma huku Duniani kwa ajili yako na mimi ili tuishi kwa huyo (**Luka 24:48-49**) hivyo ndivyo Kalvari ilimaanisha kwetu kumfuata yeye.

Kwanza, tuiangalie hiyo, kuona kile alifanya kwa ajili yetu, na sasa kile tupaswacho kufanya kwa ajili ya siku hiyo. Ni nini tunapaswa kufanya wewe na mimi? Sasa, tunasema, “Vema ninashukuru sana kwa hilo, hiyo ni nzuri sana.” Lakini tunapaswa tuikubali hiyo. Na kuikubali hiyo ni kukubali letu wa Kristo katika mioyo yetu (**Yohana 1:12-13, 17:3**).

Hapo sasa tutakuwa huru na dhambi (**Rumi 8:1-10**) kwa hiyo hakuna minyororo ya dhambi inanoning’inia kwetu hata kidogo. Ni kama vile tu hatujatenda dhambi kamwe....

(**Rumi 6:15-18, Galatia 3:15**).

Ile sadaka kamilifu ilitufanya sisi wakamilifu (**Waebrania 10:10-14**) kwa maana Yesu alisema “Iweni wakamilifu kama Baba yenu aliye Mbinguni alivyo mkamilifu” (**Mathayo 5:18**) sasa hakuna kitu cha zaidi kipaswacho kufanya, lakini tumefanywa wakamilifu uweponi pa Mungu.

Sasa hapo ndipo tunapopoteza nafasi zetu, kama hatuaangalii na tunajaribu kuangalia nyuma vile tulivyokuwa na ilimradi tunaangalia nyuma vile tulivyokuwa, ile sadaka haiwi na maana kwetu. Oh! huwezi kuliona hilo, kanisa? Sitajaribu hiyo kazi mimi siwezi, na wala wewe. Hakuna sababu ya kujaribu. Kwa kuanzia wewe ni mtu aliyepotea, ilimradi unaangalia yale uliyoyafanya. Lakini usiangalie uliyoyafanya, angalia kile ile siku pale kalvari ilivyokufanyia wewe.

Ililipa gharama yako (**1Petro 1:18-20**) ilimaliza hili swali dhambi zetu ziwe nyekundu sana zitakuwa nyeupe kama theluji. Zijapokuwa nyekundu kama bendera zitakuwa nyeupe kama sufu. (**Isaya 1:18**) kwa hiyo huna dhambi. Wewe ni kamilifu na dhambi. Haijalishi umefanya nini au unafanya nini wewe bado asiye na dhambi kabisa, ilimradi umemkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako, dhambi zako zimesamehewa, kila kilichosamehewa kimeondolewa na kusahaulika (Yeremia 31:34b). sasa unafanya nini? unakupa wewe baada ya hali hiyo, Roho wake kumfuata yeye na kufanya kama alivyofanya kwa wengine wanaomfuata yeye.

Alikuwa mtu mmoja tu, mtu mkamilifu, alitoa maisha yake, na alitoa mfano kwa ajili yako. Sasa, tunapaswa kufanya nini. Jambo la kwanza nitakalo kusema ni: Yesu kamwe hakuishi kwa ajili yake mwenyewe. Maisha yake aliyatumia kwa ajili ya wengine, hiyo ni uzima wa milele mkamilifu. Unaposema unaenda kanisani na unafanya mambo mazuri, hilo ni zuri lakini unapoishi maisha yako kwa ajili yako mwenyewe huna uzima wa milele. Uzima wa milele ni kuishi kwa ajili ya wengine (**2Kor 5:14-15, Mathayo 25:31-40**) ilithibitisha hilo alipoingia ndani ya kondoo wa Mungu (**Yohana 2:290**) aliishi na alikuwa na uzima wa milele, kwa sababu hakuishi kwa ajili yake, aliishi kwa ajili ya wengine. Na unapokea uzima wa milele unapoipokea ile siku, na hutaishi kwa ajili yako tena. Utaishi kwa jili ya wengine (**Rumi 14:7-8**). Mtu mmoja alisema “utasimamaje na kumuacha mtu akuite jina baya kama hilo?” huishi kwa ajili yako mwenyewe, unaishi kwa ajili ya wengine ili kwamba uweze kumkmbua mtu huyo (**1Yohana 5:16**) mnakuwa wana. Na shida ya hilo ni kuwa Kanisa limesahau kwamba tu wana. Ninyi ni wana (**Galatia 4:6-7**). Unachukua nafasi ya Kristo (**2Kor 5:20**) mmekuwa wana, kwa hiyo usiishi kwaajili yako, uishi kwa ajili ya wengine.

“Vema, ndugu Branham, naweza kuishi kwa ajili ya huyu ndugu kwa sababu yeye hakika ni mtu mzuri” hilo silo lenyewe. Ishi kwa aliji ya mtu Yule ambaye anakuchukia. Ishi kwa ajili ya mtu huyo ambaye anaweza kukuuwa kama anaweza. hiyo ndivyo waoivyofanya kwake, walimuua yeye, na alikufa kwamba angaweza kuwakomboa wao, huo ni uzima wa milele. Unapolipata hilo kifua au moyoni mwako, hapo sasa unaelekea mbinguni. Lakini unatoa sadaka vitu vyako mwenyewe, unavitoe kama vile kondoo atoavyo manyoya yake, unaangalia kuelekea kalvari.

Sasa, angalia kazi kubwa ilikuwa ni kuwa na nguvu katika kanisa siyo tu kuponya wagonjwa kwa maombi, na kutoa mapepo kwa maombi, lakini kuwapa watu uzima wa milele waaminio (**Yohana 14:12**) Roho Mtakatifu alikuwa anakuja na akawekwa mikononi mwa Kanisa na kuwapa uzima wa milele.oh, hivyo ndivyo Kalvari ilimaanisha.[1]

Yule Mchungaji mkuu alipopigwa, Yule kondoo mkubwa nabii alipopigwa nyuma, alisema “imekwisha” (**Yohana 19:30**) na dakika ile, mara tatu yule Mchungaji alipopigwa ilikuwa imekwisha. Dhambi ilimaliza.hakukuwa na dhambi tena. walikuwa safi, ile adhabu ililipwa.waaminio ambao majina yao yalikuwa ameandikwa katika kitabu cha uzima, waliochaguliwa kuwa mbele hata kabla ya misingi ya dunia, ilikuwa imekwisha tangu dakika ile yesu aliposema imekwisha.yeye yule Mchungaji mkuu ilikuwa imekwisha, mkono wa kuume wa Mungu ulivutwa kutoka kifua mwake, alipigwa.

Sasa siku ya pasaka (Ista) aliurudisha huo, akaufufua tena ukarudi katika kifua chake na kuunyosha chini kwangu na kwako katika umbile la neno lake, kutukomboa sisi turudi mwanzo kwenye ile bustani ambapo dhambi ilituondoa ile siri imefichwa ya ukuu wa moyo wake ilifunuliwa na nabii/ Mchungaji. Ilifunguliwa na Mchungaji, Nabii/Mchungaji.

Siyo ajabu milima iliinuka na kupiga kelele siku ile, siyo ajabu jua lilificha uso wake na kupiga kelele za furaha (**Mathayo 27:45-53**) siyo ajabu vitu vyote vya asili vilivunjika na kujiachilia, upepo ulitikisa miti ikatikisika na kutikisika na kufurahi na kuruka walimuona nabii /mchungaji pale mlimani akikomboa kila jina katika kitabu cha uzima. Na walio asili yao wenyewe imekombolewa. Walilia na kuruka na Dunia ilingia katika tetemeko, na milima ilipasuka, na mawe yakaanguka, na jua likatiwa giza, na kila kitu kikatulia, kama mkutano mwingine wa kati yule Mchungaji aliyefunua ya kuwa “imekwisha” [2]

Mungu alipouangalia ule mwili..... Roho alikuwa amemuacha yeye, pale bustani ya Gethemane. Ilibidi afe, kama mtu (**Yohana 19:25-30**). Kumbukeni marafiki, hakulamiza kufanya hivyo .huyo alikuwa Mungu , Mungu ameupaka mafuta huo mwili , ambao ulikuwa wa kibinadamu (**Rumi8:3-4**). Kama angelienda pale kama mungu asingeweza kamwe kufa kifo kama kile, lakini kumbuka alienda pale pamoja na wewe ukiwa ndani yake. Unaona , Mungu bado hajamtenganisha bibi arusi na bwana arusi nab ado, kwa hiyo Mungu alipoangalia mwili wa Yesu Kristo, aliwaona wote bwana na bibi, vyote vilikombolewa katika ule mwili mmoja. Unaona? wao ni mmoja , sawa , neno lilelile, neno lilelile lililozungumzwa juu ya Bwana arusi. Linazungumza juu ya Bibi arusi!.

Vema ni kwa namna gani Bibi harusi anakuja na shindwe kudhihirisha kila kitu kilichokuwa kimeahidiwa juu ya yeye. Na yule Bwana harusi, akaja na yeye asingekuwa Bibi harusi? lakini alipokwisha kufanya yote, hata kwa kujiinua mwenyewe kutoka kwa wafu, baadae hapo si ni lazima Bibi harusi afanye jambo lile, iwe ni vile neno limesema yeye atakuwa katika siku hizi za mwisho? Je hanazo sika za Sodoma? Je Dunia si inabidi iwe kama Sodoma? si ni lazima Dunia iwe kama vile hasa ilivyoko, je mambo hayo si makamilifu kabisa, je mambo hayo si utambulisho mkamilifu wa neno la Mungu likielezwa kwetu?

Lakini Mungu aliona kimbele yule Bibi harusi akiwa ndani ya Bwana harusi. Hallelujah! Unaona, kumuokoa mke wake, kuwa kama Adamu, ilibidi aende pamoja naye, Adamu alijua kile alichokuwa anaenda kukifanya . hawa hakujua kile alichokuwa anafanya . Lakini Adamu alitoka nje pamoja na mke wake. Unaona? na Yesu alichukua nafasi ya mkewe unaona? naYesu alichukua nafasi yake wake naye akafanyika kuwa dhambi kwa ajili yake kumbuka. Alifanyika wewe, alistahimili hukumu yako, ili kwamba uweze kusimama mahali pake, ni upendo wa jinsi gani! Ushirika wa jinsi gani! Tunawezaje kulikataa hilo? Twawezaje kufanya jambo linginelo zaidi ya kumpenda yeye, marafiki? [3]

## **Nukuu za kingereza**

[1] “Siku ile pale kalvari” (60-0925) uk 7-8, 14-19.

[2] “Kwa nini ilikuwa wachungaji” (64-1221) aya 181-182.

[3] “Ni kule kuchomoza kwa jua” (65-0418M) uk.34-35.

---

□□□□□□□□□□□□□□ **LA KUJENGEA NA 4** kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii. Iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69-D– 75328 Schomberg Germany Simu (+49) 7235 - 7613. Fax (+49) 7235 3306.

---

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia, zile mbegu zitaingizwa magazetini na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi za kiingereza na kiswahili. Andika kwa: Charles E. Y. Kanju*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*